UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM
COMPUTING CENTRE

TAARIFA KWA UMMA

1. Utangulizi:

Kitengo cha Kompyuta cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, maarufu kama University of Dar es Salaam Computing Centre (UCC), ni kampuni inayomilikiwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) na kusajiliwa na Ofisi ya Msajili wa Makampuni mwaka 2001 kwa hati ya usajili namba 40718. Lengo la UCC ni kutoa huduma na ushauri kwenye tasnia ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kwa CKD na kwa wateja wa nje kwa mfumo wa kibiashara. Huduma zinazotolewa na UCC ni pamoja na utengezaji wa mifumo ya kompyuta (*software),* usanifu, uwekaji na usimamiaji wa miundombinu ya TEHAMA na kutoa mafunzo na huduma za ushauri katika tasnia ya TEHAMA. UCC ina menejimenti yake, Bodi ya Wakurugenzi na inawajibika kwa CKD kupitia kwenye mkutano mkuu wa wanahisa (*Annual General Meeting).*

Hivi karibuni kumekuwa na taarifa mbalimbali kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ambazo zinapotosha ukweli kuhusu uendeshaji wa UCC na hali ya kibiashara ya Kampuni. Kutokana na hali hiyo, Bodi ya Wakurugenzi ya UCC katika Kikao chake cha 79 kilichofanyika tarehe 28/9/2018 imeona ni vyema kuufahamisha umma kuhusu hali halisi ya UCC ikiwa ni pamoja na changamoto mbalimbali za uendeshaji inazopambana nazo na hatua zinazochukuliwa kukabili changamoto hizo ili kuongeza ufanisi wa kibiashara wa Kampuni.

2. Hali ya Utendaji wa Kampuni na Hatua Zilizochukuliwa

Katika kipindi cha kujiendesha kama kampuni, UCC imekuwa na matokeo yanayobadilika kutoka kipindi kimoja hadi kingine. Kwa miaka ya karibuni, UCC imekuwa na matokeo yasiyoridhisha kibiashara huku idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika kozi zake mbali mbali ikishuka hivyo kupunguza mapato ya Kampuni kupitia ada. Mahesabu yaliyokaguliwa yanaonesha kuwa katika kipindi cha miaka minne (2011/2012 – 2014/2015) UCC ilipata faida katika mwaka mmoja tu huku ikijilimbikizia kiasi kikubwa cha hasara. Kwa upande wa biashara ya mafunzo, mapato yamepungua kwa asilimia 56 au wastani wa asilimia 11 kwa mwaka kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 mpaka 2017/2018. Vile vile kiwango cha tija na maslahi kwa wafanyakazi vilikuwa chini.

Kwa kuwa UCC inatakiwa kujiendesha kibiashara bila kupokea ruzuku yeyote, Bodi ya Wakurugenzi, na CKD viliona umuhimu wa kupanga na kutekeleza mikakati mbalimbali ili kurekebisha hali ya utendaji. Lengo si tu kuhakikisha UCC inajiendesha kibiasharabali pia kutoa huduma bora kwa CKD na wateja wengine, pamoja na kuwa na tija na ufanisi katika utendaji. Mikakati na hatua ambazo zimechukuliwa na Menejimenti ya UCC kwa usimamizi wa Bodi ya Wakurugenzi wa UCC ni pamoja na:

(i). **Kufanya Ukaguzi wa rasilimali watu (*Human Resource Audit*):** Zoezi hili lilifanyika Agosti, 2015 kwa kulinganisha ikama na weledi/ujuzi unaohitajika na ule uliopo, kubaini upungufu uliopo na kuweka mikakati ya kukabiliana na upungufu uliobainika.

(ii). **Kupitia sera ya motisha kwa wafanyakazi (Incentive and Bonus scheme):** Sera hii ililenga katika kuongeza tija, mapato na faida. Hivi vingefikiwa kwakuboresha masilahi ya wafanyakazi na malengo ya Kampuni kwa kuoanisha malipo na utendaji kazi wa mfanyakazi pamoja na kuwapa motisha wafanyakazi wanaojiendeleza kiujuzi.

(iii). **Kupitia Muundo wa Utumishi (*Scheme of Service*):** Lengo la zoezi hili ilikuwa kuweka uwiano baina ya wafanyakazi wa kada moja ili kuleta ulinganifu wa mishahara na vyeo kwa wafanyakazi wote wanaolingana sifa, muda waliokaa kazini (*seniority*)na majukumu ili kuondoa malalamiko ya siku nyingi ya upendeleo na hivyo kuwaongezea motisha na weledi katika utendaji kazi wao. Muundo mpya ulianza kutekelezwa Julai 1, 2016.

(iv). **Kupitia Mpango Mkakati na kutengeneza Mpango Mkakati mpya wa 2016/2017 mpaka 2020/2021 (*Revised Strategic Plan*)**: Mpango Mkakati huu ulilenga kuwa na kampuni inayojiendesha kwa faida kwa kuandaa na kutoa huduma za TEHAMA zenye ubora wa juu; kupata na kuendelea kuwa na wateja wenyekuridhika na huduma zitolewazo na Kampuni; na kuajiri na kuhifadhi (*retain*) wafanyakazi weledi na walioridhika. Mkakati mpya ulianza kufanya kazi kuanzia Julai 2016.

(v). Kupunguza gharama za Uendeshaji: Hatua hii ililenga katika maeneo makuu mawili: Kodi ya majengo yaliyopangishwa na UCC kwa ajili ya kuendesha shuguli zake na gharama za pamoja za uendeshaji (*central overheads*).

a) Kupunguza kodi ya majengo (ambayo nigharama isiyobadilika – *fixed costs*) kulihusisha kuhama kutoka kwenye majengo yenye gharama kubwa, kupunguza maeneo inayopangisha ili kuendana na hali halisi ya biashara na pia, kwa kadiri inavyowezekana, kuingia mikataba kwa kutumia shilingi ya Kitanzania badala ya fedha za kigeni. Mkakati huu, ambao pia unaendana na maelekezo ya Serikali kwa taasisi zake kuhamishia shughuli zake kwenye majengo ya umma, umepunguza kodi ya pango kutoka karibu TZS 1.5 bilioni kwa mwaka wa 2014/2015 mpaka chini ya TZS 400 milioni kwa mwaka wa 2018/2019.

b) Menejimenti imechukua hatua mbali mbali kuepuka gharama zisizokuwa ambazo. Hatua hizi zimepelekea kupungua kwa gharama za pamoja za uendeshaji (*central overheads*) kutoka kama TZS 2.468 billioni mwaka 2014/2015 mpaka chini ya TZS 1 billioni 2017/2018.

Izingatiwe kuwa Bodi ya Wakurungezi imekuwa inataarifiwa na Menejimenti ya UCC kuhusu hatua na mikakati hii na kutoa ushauri, ridhaa na kupitisha kwa kadiri ilivyohitajika.

3. Kurekebisha Muundo wa Biashara na Kujenga UCC Mpya

Katika kutekeleza Mpango Mkakati wa 2016/2017 mpaka 2020/2021 UCC imefanya tathimini ya kina ya uendeshaji na ufanisi wa kibiashara kwa aina za biashara na huduma zinazotolewa na Kampuni. Tathmini hii iliwasilishwa na kuridhiwa na Bodi ya Wakurugenzi katika kikao chake cha 77 kilichofanyika tarehe 04/05/2018 pamoja na Mkutano Mkuu wa 14 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 17/05/2018. Kwa tathmini hii UCC imeandaa na inatekeleza Mpango wa Kurekebisha Muundo wa Kibiashara ambao umelenga kuifanya UCC ioanishe shughuli zake na malengo makuu ya CKD na ya taifa kwa ujumla.

Kibiashara, mpango huu unapelekea mabadiliko makubwa katika sehemu mbili:

(i). Kwanza, kuimarisha biashara za utengenezaji wa mifumo ya kompyuta (*software*) na Miundombinu ya TEHAMA (ICT infrastructure). Nyanja hizi za biashara hii siyo tu zimekuwa na matokeo mazuri ya kibiashara katika siku za karibuni bali pia zimekuwa na uhitaji mkubwa kwa CKD na serikali na taasisi zake. Kwa miaka mitatu iliyopita UCC imefanya kazi za software na miundombinu kwa taasisi mbalimbali zikiwemo CKD, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

(ii). Pili, kurekebisha biashara ya mafunzo na utumiaji wa rasilimali zilizoko katika matawi. Marekebisho haya yanalenga kubadilisha aina ya mafunzo yanayotolewa na UCC kwa kuhuisha mitaala yake na rasilimali watu inayofundisha mitaala hiyo na mahitaji ya soko na mabadiliko katika tasnia ya TEHAMA nchini na duniani kote. Marekebisho haya yatagusa kozi za kitaaluma (*academic courses*) na mafunzo ya weledi (*professional courses*).

a) Kwa kozi za kitaaluma, UCC inajikita katika kutengeneza na kuendesha kozi zinazolenga kwenye ujuzi wa moja kwa moja (*hands-on skills*). Hii imeanza kwakupitia na kurekebisha mitaala ya kufundishia (*review of teaching curriculum*) pamoja na kuoanisha biashara ya mafunzo na biashara nyingine za software na mifumo kwa kutoa fursa kwa wanafunzi kupata mafunzo kwa vitendo kwenye idara hizi.

b) Kwa upande wa kozi za weledi (*professional courses*) UCC inaangalia malengo na miongozo ya serikali kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi katika ngazi ya juu ikiwa ni pamoja na yale yanayohusiana na vyeti vya weledi (*professional certification*). Hadi sasa UCC imefanikiwa kuendesha mafunzo kwa tasisi mbalimbali ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania, na kwa watumishi wa serikali kutoka maeneno mbalimbali kwa usimamizi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kiuendeshaji, Mpango wa Kurekebisha Muundo wa Kibiashara, unagusa mambo makubwa matatu: sehemu ambazo huduma za UCC zitakuwa zinatolewa; utumiaji wa rasilimali na idadi ya wafanyakazi.

(i). Kutokana na upembuzi wa kina kibiashara, mpango huu utapelekea kufungwa kwa matawi ambayo yamekuwa yakijiendesha kwa hasara. Matawi hayo ni Arusha (litafungwa Octoba 2018), Mwanza (litafungwa Machi 2019) na Mbeya (litafungwa Septemba 2019). Hii itapelekea UCC kubakiwa na matawi matatu yaani Makao Makuu (yaliyoko CKD), City Centre (Dar es Salaam) na Dodoma. Tawi la Dodoma

3. Kurekebisha Muundo wa Biashara na Kujenga UCC Mpya

Katika kutekeleza Mpango Mkakati wa 2016/2017 mpaka 2020/2021 UCC imefanya tathimini ya kina ya uendeshaji na ufanisi wa kibiashara kwa aina za biashara na huduma zinazotolewa na Kampuni. Tathmini hii iliwasilishwa na kuridhiwa na Bodi ya Wakurugenzi katika kikao chake cha 77 kilichofanyika tarehe 04/05/2018 pamoja na Mkutano Mkuu wa 14 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 17/05/2018. Kwa tathmini hii UCC imeandaa na inatekeleza Mpango wa Kurekebisha Muundo wa Kibiashara ambao umelenga kuifanya UCC ioanishe shughuli zake na malengo makuu ya CKD na ya taifa kwa ujumla.

Kibiashara, mpango huu unapelekea mabadiliko makubwa katika sehemu mbili:

(i). Kwanza, kuimarisha biashara za utengenezaji wa mifumo ya kompyuta (*software*) na Miundombinu ya TEHAMA (ICT infrastructure). Nyanja hizi za biashara hii siyo tu zimekuwa na matokeo mazuri ya kibiashara katika siku za karibuni bali pia zimekuwa na uhitaji mkubwa kwa CKD na serikali na taasisi zake. Kwa miaka mitatu iliyopita UCC imefanya kazi za software na miundombinu kwa taasisi mbalimbali zikiwemo CKD, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

(ii). Pili, kurekebisha biashara ya mafunzo na utumiaji wa rasilimali zilizoko katika matawi. Marekebisho haya yanalenga kubadilisha aina ya mafunzo yanayotolewa na UCC kwa kuhuisha mitaala yake na rasilimali watu inayofundisha mitaala hiyo na mahitaji ya soko na mabadiliko katika tasnia ya TEHAMA nchini na duniani kote. Marekebisho haya yatagusa kozi za kitaaluma (*academic courses*) na mafunzo ya weledi (*professional courses*).

a) Kwa kozi za kitaaluma, UCC inajikita katika kutengeneza na kuendesha kozi zinazolenga kwenye ujuzi wa moja kwa moja (*hands-on skills*). Hii imeanza kwakupitia na kurekebisha mitaala ya kufundishia (*review of teaching curriculum*) pamoja na kuoanisha biashara ya mafunzo na biashara nyingine za software na mifumo kwa kutoa fursa kwa wanafunzi kupata mafunzo kwa vitendo kwenye idara hizi.

b) Kwa upande wa kozi za weledi (*professional courses*) UCC inaangalia malengo na miongozo ya serikali kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi katika ngazi ya juu ikiwa ni pamoja na yale yanayohusiana na vyeti vya weledi (*professional certification*). Hadi sasa UCC imefanikiwa kuendesha mafunzo kwa tasisi mbalimbali ikiwemo Benki Kuu ya Tanzania, na kwa watumishi wa serikali kutoka maeneno mbalimbali kwa usimamizi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kiuendeshaji, Mpango wa Kurekebisha Muundo wa Kibiashara, unagusa mambo makubwa matatu: sehemu ambazo huduma za UCC zitakuwa zinatolewa; utumiaji wa rasilimali na idadi ya wafanyakazi.

(i). Kutokana na upembuzi wa kina kibiashara, mpango huu utapelekea kufungwa kwa matawi ambayo yamekuwa yakijiendesha kwa hasara. Matawi hayo ni Arusha (litafungwa Octoba 2018), Mwanza (litafungwa Machi 2019) na Mbeya (litafungwa Septemba 2019). Hii itapelekea UCC kubakiwa na matawi matatu yaani Makao Makuu (yaliyoko CKD), City Centre (Dar es Salaam) na Dodoma. Tawi la Dodoma

halijafanya vizuri kibiashara katika miaka iliyopita. Hata hivyo Dodoma ni eneo la kimkakati kwa UCC hasa ukizingatia kuwa Serikali sasa imehamishia rasmi makao yake makuuhuko. Hatua zinachukuliwa kwa kuliongezea tawi rasilimali watu na vifaa kutoka katika matawi yanayofungwa.

(ii). Kuongeza ufanisi katika utumiaji rasilimali watu na rasilimali nyingine itafanyika kwa kuhamisha rasilimali hizi kutoka matawi yanayofungwa kwenda katika matawi yanayobaki. Hii itaendana na kufanyia ukarabati (refurbishment) vifaa vitakavyohamishwa ili kuboresha mazingira na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

(iii). Uwezekano wa kupunguzwa kwa baadhi ya wafanyakazi ili kuoanisha biashara na muundo wa uendeshaji kwa upande mmoja na ikama na weledi kwa upande mwingine. Kwa kuwa zoezi la kupunguza wafanyakazi hufanyika kulingana na sheria na taratibu za nchi, Menejimenti ilitoa Notisi ya Kusudio la Kupunguza Wafanyakazi mwezi Juni 2018. Pia Menejimenti imeanza kufanya majadiliano na chama cha wafanyakazi wa taasisi za elimu ya juu (THTU) ambacho kina wanachama ndani ya UCC. Mpaka sasa vikao vitatu vimeshafanyika na majadiliano bado yanaendelea.

4. Hitimisho

Bodi ya Wakurugenzi ya UCC inaamini kuwa hatua mbali mbali zilizochukuliwa kwa miaka mitatu iliyopita, zinalenga na zitaweza kuigeuza UCC kuwa taasisi inayojiendesha kibiashara na inayotoa mchango mkubwa katika malengo makuu ya CKD na taifa kwa ujumla. Pia hatua zote zilizochukuliwa zimefuata taratibu na sheria pale inapobidi, ikiwa ni pamoja na kupata ridhaa ya CKD ambaye ndiye mmiliki.

Bodi ya Wakurugenzi ya UCC inapenda kuwahakikishia wateja wetu, wadau wengine na umma kwa ujumla kuwa bado inaendelea kutoa huduma zake na hatua zinazochukuliwa zina lengo la kuboresha huduma hizo katika hali endelevu. UCC inathamini mchango na ushirikiano inaoupata kutoka kwa wateja, wadau na umma kwa ujumla katika kuipeleka mbele.

Imetolewa na

Profesa Makenya A. H Maboko
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi
UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM COMPUTING CENTRE
Tarehe 1 Oktoba 2018